# Mwongozo wa Usaidizi wa Nyumba wa Idaho

## Nyenzo na desturi bora kwa wale wanaotafuta nyumba ya kupangisha

**www.housingidaho.com / www.viviendaidaho.com**

| |
|---|
| ***Tafadhali Kumbuka:*** *Mipango, nyenzo na maelezo ya mawasiliano yaliyo katika mwongozo huu yanaweza kubadilika; rejelea toleo la mtandaoni kwenye housingidaho.com/HousingAssistanceGuide kwa taarifa za sasa. Mwongozo huu si mkamilifu na unatolewa tu kama sehemu ya kuanzia na utangulizi wa aina maarufu za nyumba na usaidizi husika. Nyenzo na huduma zinategemea matakwa ya ustahiki ya serikali kuu na/au upatikanaji wa fedha.* |
| *Wasilisha masahihisho au masasisho kwenye hirc@ihfa.org.*<br>*Mara ya Mwisho Ilisasishwa:* 17/06/2024 |

# Maudhui


**Utangulizi** .... 1

**Aina za Nyumba** .... 1

**Aina za Usaidizi wa Nyumba** .... 2

- **Vocha ya Chaguo la Nyumba (Sehemu ya 8)** .... 2
- **Nyumba ya ruzuku** .... 2
- **Kifungu cha 42 au Ghorofa za Mkopo wa Ushuru wa Nyumba kwa Walio na Mapato ya Chini** .... 2

**Kile ambacho wapangaji wote wanapaswa kujua** .... 3

- **Mapendekezo ya msingi** .... 3
- **Sheria za Nyumba zenye usawa hukulinda** .... 3

**Jinsi ya kupata nyumba ya kupangisha kwenye housingidaho.com** .... 4

**Jinsi ya kutuma ombi la nyumba ya kupangisha** .... 5

- **Nyumba za viwango vya soko** .... 5
- **Nyumba ya ruzuku** .... 5

**Umechelewa kulipa kodi ya mwezi huu?** .... 5

**Unachelewa Kulipa Kodi Mara kwa Mara?** .... 5

**Je, Unapitia Dhuluma za Nyumbani au Unyanyasaji wa Kimapenzi?** .... 5

**Uko kwenye hatari ya kufukuzwa kwenye nyumba au kupoteza makao?** .... 6

**Nyenzo** .... 6

- **Ukanda 1** .... 7
- **Ukanda 2** .... 7
- **Ukanda wa 3** .... 7
- **Ukanda 4** .... 7
- **Ukanda 5** .... 7
- **Ukanda 6** .... 7
- **Ukanda 7** .... 7

## Utangulizi

Masuala ya uchumi na ajira pamoja na janga la COVID-19 yamewaacha wakazi wengi wa Idaho bila nyumba thabiti. Ingawa kuna changamoto nyingi, kumbuka vitu hivi vinne:

- **Tafuta usaidizi mapema.** Usisubiri kufukuzwa kwenye nyumba wala mali yako kuchukuliwa ili kupata machaguo na kutuma maombi.
- **Kuwa na uwezo wa kubadilika.** Upungufu wa nyumba katika jimbo la Idaho unapunguza machaguo. Hifadhi zinaweza kuwa hatua ya kwanza ya kurudi kwenye nyumba na uthabiti.
- **Makinika na upate vidokezo.** Hifadhi majina ya watu wa kuwasiliana nao na nambari na uulize jinsi unavyopaswa kufuatilia. Hakikisha kuwa watoaji wa nyumba au huduma wanajua jinsi ya kuwasiliana nawe inapohitajika.
- **Songa mbele kwa mpango.** Pindi unaposhughulikia mahitaji ya haraka, unda mpango wa muda mrefu. Ingia kwenye orodha za wanaosubiri nyumba za kupangisha za gharama ya chini na usaidizi mwingine. Usiruhusu orodha za wanaosubiri kukuzuia kutuma ombi la usaidizi.

Nyenzo na mipango iliyoorodheshwa katika mwongozo huu zimefafanuliwa na Kanda katika jimbo zima la Idaho. Rejelea ramani hapa chini ili uone kaunti zilizojumuishwa katika kila Ukanda:




| Ukanda | Kaunti |
|---|---|
| Ukanda 1 | Benewah, Bonner, Boundary, Kootenai, Shoshone |
| Ukanda 2 | Clearwater, Idaho, Latah, Lewis, Nez Perce |
| Ukanda wa 3 | Adams, Boise, Canyon, Elmore, Gem, Owyhee, Payette, Valley, Washington |
| Ukanda 4 | Blaine, Camas, Cassia Gooding, Jerome, Lincoln, Minidoka, Twin Falls |
| Ukanda 5 | Bannock, Bear Lake, Bingham, Caribou, Franklin, Oneida, Power |
| Ukanda 6 | Bonneville, Butte, Clark, Custer, Fremont, Jefferson, Lemhi, Madison, Teton |
| Ukanda 7 | Ada |

## Aina za Nyumba

**Hifadhi ya Dharura:** Hifadhi ya muda mfupi kwa watu binafsi na familia.

**Nyumba za Mpito:** ‘Suluhu’ ya muda mfupi kwa nyumba thabiti zaidi.

**Ya ruzuku au Malipo yanayopungua:** Kodi inategemea asilimia ya mapato ya jumla ya familia.

**Nafuu:** Kodi isiyobadilika, lakini mara nyingi ni chini ya nyumba ya viwango vya soko.

**Kiwango cha soko:** Hakuna usaidizi wa fedha.

**Nyumba ya Usaidizi:** Ni msamiati maarufu unaoelezea nyumba na huduma za usaidizi kwa wapangaji wakongwe/walemavu.

# Aina za Usaidizi wa Nyumba

## Vocha ya Chaguo la Nyumba (Sehemu ya 8)

Vocha zinapewa wapangaji wanaostahiki. Familia zinalipa asilimia 30 ya mapato kwa kodi.

***Bora kwa:*** Mapato yasiyobadilika (SSI, Ulemavu) au mapato ya nyumba kwenye au chini ya asilimia 30 ya Mapato Wastani ya Eneo.

***Faida:*** Vocha inaweza kuhamishwa nje ya kaunti ilikotengewa na mpangaji anachagua aina na eneo la nyumba. Usaidizi unalingana na mpangaji.

***Hasara:*** Muda wa orodha ya wanaosubiri ni wastani wa miezi 12-18.

***Jinsi ya kutuma ombi la Vocha ya Chaguo la Nyumba (HCV)***

**Kaunti ya ADA (Ukanda wa 7)** Boise City/Ada County Housing Authority (bcacha.org). Tuma ombi mtandaoni hapa au piga simu 208-345-4907.

**Kaunti za CANYON, OWYHEE, ELMORE, GEM, PAYETTE, ADAMS, VALLEY AU WASHINGTON** Southwest Idaho Cooperative Housing Authority (sicha.org). Tuma ombi mtandaoni hapa au piga simu 208-585-9325.

**Kaunti NYINGINE ZOTE** Idaho Housing and Finance Association (IHFA) hutoa mpango wa HCV kwa kaunti 34 zilizosalia. Tembelea idahohousing.com/rental-assistance/rental-assistance-application/ ili uanze ombi lako la mtandaoni au piga simu kwenye ofisi ya tawi iliyo karibu nawe:

- **Ukanda wa 1** Coeur d'Alene Branch Office, 208-762-5113
- **Ukanda wa 2** Lewiston Branch Office, 208-743-0251
- **Ukanda wa 4** Twin Falls Branch Office, 208-734-8531
- **Ukanda wa 5/6** Idaho Falls Branch Office, 208-522-6002

*Kidokezo: Tafuta mawasiliano kutoka kwenye mamlaka ya nyumba na ujibu haraka kila wakati. Wasiliana na mamlaka ya nyumba angalau kila miezi 3 hadi 4 ili kuangalia hali yako, au wakati wowote unapobadilisha nambari ya simu au anwani yako.*

## Nyumba ya ruzuku

Pia huitwa usaidizi wa 'malipo yanayopungua' ya mradi,' ghorofa hizi zina nyumba fulani za familia zilizo na mapato ya chini sana.

***Bora kwa:*** Wale walio kwenye orodha za wanaosubiri sasa za Housing Choice Voucher; yeyote anayetimiza miongozo ya Mpango wa HCV.

***Faida:*** Hakuna vocha inayohitajika.

***Hasara:*** Ghorofa pekee. Usaidizi unasalia kwenye ghorofa, hauhamishwi (kubebeka). Orodha za wanaosubiri zinatofautiana kulingana na eneo.

***Jinsi ya kutuma ombi****:* Wasiliana na meneja wa ghorofa ili kuamua nafasi na ustahiki kisha uwasilishe ombi.

## Kifungu cha 42 au Ghorofa za Mkopo wa Ushuru wa Nyumba kwa Walio na Mapato ya Chini ***(tafuta housingidaho.com)***

Kodi hazibadiliki na ni nafuu kwa familia zilizo na mapato yanayolingana na mshahara wa kazi ya muda kamili kwa au chini ya $20 kwa saa.

***Bora kwa:*** Familia zilizo na mapato ya chini hadi wastani.

***Faida:*** Nyumba nyingi zilizopo na majumba mapya. Itakubali Vocha za Housing Choice *(Vocha za HCV)*.

***Hasara:*** Ghorofa pekee. Kodi zisizobadilika si nafuu kwa kila mtu.

***Jinsi ya kutuma ombi:*** Wasiliana na meneja wa ghorofa na ukamilishe ombi.

| Kile ambacho wapangaji wote wanapaswa kujua |
|---|
| Mapendekezo ya msingi |
| ***Eneo.*** Inapowezekana, tafuta nyumba karibu na mahali pa kazi, shule, au eneo jingine muhimu. Gharama za usafiri zinaweza kuongeza zaidi gharama yako ya maisha kwa jumla. |
| ***Huduma za msingi.*** Ikiwa huduma za msingi hazijajumuishwa katika kodi, omba uone gharama za wastani za huduma za msingi za majira ya joto na baridi. |
| ***Marekebisho ya ufikiaji.*** Tafuta nyenzo kwenye idahoat.org/resources/at-disability > Marekebisho ya nyumbani |
| ***Mkataba wa kupangisha nyumba.*** Hakikisha kuwa umeelewa mkataba wa kupangisha nyumba na gharama zote kabla ya kutia sahihi chochote. Ikiwa una maswali, mwombe mtu unayemwamini akusaidie kupitia waraka wowote. Omba mkalimani au mtafsiri inapohitajika. |
| ***Orodha za Wanaosubiri.*** Unaweza kuwa kwenye orodha kadhaa za wanaosubiri, lakini huenda ukahitajika kulipa ada ya ombi kwa kila orodha. |
| **Jilinde kutokana na udanganyifu!** Wahalifu wanachukua pesa za nyumba ambazo hawana haki ya kupangisha. Angalia ishara za udanganyifu na ujilinde. Pata maelezo zaidi hapa. Ikiwa linaonekana jambo la kutilia shaka, amini hivyo. |
| **Fahamu haki na majukumu yako** na usome mikataba yote ya kupangisha nyumba kwa makini kabla ya kutia sahihi. Unaweza kuomba nakala ya "Haki za Mpangaji" kutoka kwenye ofisi yako ya tawi la karibu la Idaho Legal Aid Services au piga simu kuu kupitia (208) 746-7541. |
| **Jadili.** Usiogope kujadili ikiwa unahitaji badiliko kwenye mkataba wa kupangisha nyumba. Fanya mabadiliko au makubaliano kwa njia ya maandishi, kisha utii makubaliano hayo. |
| **Kuwa mwaminifu.** Kuwa tayari kuonyesha kwamba unaweza kutimiza matakwa ya mkataba wa kupangisha nyumba na uwe mpangaji wa kuwajibika. Kuwa mwaminifu siku zote kwa mwenye nyumba ili kuepuka matatizo baadaye. |
| **Kuwa na heshima na ulipe wakati unaofaa**. Wenye nyumba au meneja wa nyumba huwathamini wapangaji wanaoheshimu nyumba na wapangaji wengine, na wale wanaolipa wakati unaofaa. Uchunguzi wa ripoti ya mikopo na marejeleo ya kukodi nyumba huwasaidia kuelewa utendaji wako wa zamani katika sehemu hizi. |

| Sheria za Nyumba zenye usawa hukulinda |
|---|
| Sheria za Nyumba zenye usawa hutumika kwa mauzo ya nyumba, upangaji, ufadhili na utangazaji. Ikiwa unadhani kuwa wewe ni mwathiriwa wa ubaguzi kulingana na tabaka linalolindwa (mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsia, hali ya ndoa au ulemavu), wasiliana na yeyote kati ya wafuatao kwa maelezo zaidi au wasilisha malalamishi: **Idaho Care Line** 2-1-1; **HUD Fair Housing Line**, 1-800-877-0246 or **Intermountain Fair Housing Council**, 1-800-717-0695 |
| Ikiwa una ulemavu unaozuia zaidi shughuli kubwa moja au zaidi za maisha, unaweza kuomba marekebisho au mabadiliko yanayofaa. Hii inaweza kuhusisha marekebisho ya muundo (mfano ngazi ya kiti cha magurudumu) au makazi (kama vile uwezo wa kukaa na mnyama wa usaidizi au kutumia nafasi ya maegesho yaliyotengwa). Kwa maelezo zaidi, tembelea https://www.hud.gov/ au wasiliana na mashirika yaliyoorodheshwa hapo juu. |

# Jinsi ya kupata nyumba ya kupangisha kwenye [housingidaho.com](housingidaho.com)

1-877-428-8844

Bofya kitufe cha ***'Tafuta Nyumba za Kupangisha'*** na uteue jiji au kaunti ili kutafuta. Pia unaweza kuandika jiji, kaunti au msimbo wa eneo katika nafasi ya kutafuta.




Katika kidirisha cha ***'Machaguo ya Utafutaji Nyumba'***, weka idadi ya vyumba vya kulala unavyohitaji, kodi unayoweza kumudu na vichujio vingine vyovyote vya hiari, kisha ubofye *'Tafuta'*. Bofya vichupo vya 'Juu Zaidi' na 'Ufikiaji' ili kuboresha zaidi utafutaji wako.




Ukurasa utaonekana ukionyesha orodha za nyumba za kupangisha za karibu. Unaweza kuonyesha kwenye ramani na uchapishe orodha hii ikihitajika.

# Jinsi ya kutuma ombi la nyumba ya kupangisha

Pindi unapopata orodha inayofaa mahitaji yako na bajeti yako, wasiliana na meneja wa nyumba kwa ajili ya kutuma ombi.

Nyumba za viwango vya soko

Wenye nyumba wengi wanahitaji uchunguzi wa mikopo na ada ya ombi isiyorejeshwa, kwa hivyo kuwa tayari kulipa $15-$50 kwa kila mtu mzima katika familia. Utahitaji nyaraka hizi:

- Kitambulisho cha picha (kitambulisho cha jimbo au leseni ya udereva)
- Uthibitishaji wa mapato (kama vile hati ya malipo)
- Warejelewa wa kupangisha (meneja wa kesi, mwenye nyumba wa zamani, mwajiri, n.k.)

Nyumba ya ruzuku

Hakuna ada ya maombi. Huenda ukahitaji kuleta nyaraka zifuatazo au hati sawa:

- Kadi ya I-94 (nakala ya mbele na nyuma) kwa kila mwanafamilia
- Kadi ya Ruzuku ya Serikali ya kila mwanafamilia na vyeti vya kuzaliwa vya kila mtoto aliyezaliwa Marekani.
- EAD (Waraka wa Idhini ya Ajira) au Kadi ya Mkazi wa Kudumu
- Kitambulisho cha jimbo au leseni ya udereva
- Uthibitishaji wa mapato na warejelewa wa kupangisha (meneja wa kesi, mwenye nyumba wa zamani, mwajiri, n.k.).

**Baada ya kutuma ombi**

Angalia ujumbe wa maandishi, notisi za barua pepe au barua kutoka kwa mmiliki au meneja wa nyumba na kujibu haraka siku zote. Wasiliana na meneja angalau kila miezi sita ili kuangalia hali yako.

## Umechelewa kulipa kodi ya mwezi huu?

Zungumza na mwenye nyumba wako na ujadili ratiba ya malipo kisha utii makubaliano.

Pata ushauri wa kodi wa bila malipo kutoka kwa washauri wa nyumba walioidhinishwa wa HUD kwenye IHFA. Piga simu, 877-695-2655 au wasilisha fomu mtandaonihapa.

Wasiliana na Access Point ya kanda iliyo karibu. Tembelea idahohousing.com/homeless-resources ili upate Access Point iliyo karibu nawe.

## Unachelewa Kulipa Kodi Mara kwa Mara?

Pitia bajeti yako ya familia na upunguze uharibifu au gharama zisizo muhimu. Lipa kodi kwanza ili kuepuka kufukuzwa.

Zungumza na mwenye nyumba wako ili kuona ikiwa anaweza kushirikiana nawe.

Pata nyumba ya kupangisha ya gharama ya chini kwenye **housingidaho.com**, 1-877-428-8844

Tafuta usaidizi wa chakula, huduma za msingi au gharama nyingine katika jamii yako kwa kuwasiliana kupitia Simu ya Idaho Care, 2-1-1 au Community Action Partner, 877-375-7382

Pata ushauri wa kodi wa bila malipo kutoka kwa washauri wa nyumba walioidhinishwa wa HUD kwenye IHFA. Piga simu, 877-695-2655 au wasilisha fomu mtandaonihapa.

## Je, Unapitia Dhuluma za Nyumbani au Unyanyasaji wa Kimapenzi?

***Ikiwa uko kwenye hatari, piga 9-1-1***

**Pigia Idaho Domestic Violence Hotline** kwa 1-800-669-3176 au tembelea idvsa.org kwenye kompyuta salama.

**Tembelea idahohousing.com/homeless-resources** ili uone Hifadhi za Dhuluma za Nyumbani na nambari za simu za dharura za saa 24 katika Ukanda wako.

## Uko kwenye hatari ya kufukuzwa kwenye nyumba au kupoteza makao?

***Ikiwa uko kwenye hatari, piga 9-1-1***

***Wasiliana na Access Point*** ili kuzungumza na mtu kuhusu matatizo yako ya nyumba na kugundua nyenzo zilizopo katika Ukanda wako. Tembelea idahohousing.com/homeless-resources ili uone taarifa zaidi kuhusu Access Point iliyo karibu nawe.

- **Ukanda 1:** St. Vincent De Paul of North Idaho, 208-664-3095
- **Ukanda 2:** Sojourners' Alliance, 208-310-4554
- **Ukanda wa 3:** CATCH of Canyon County, 208-495-5688
- **Ukanda 4:** South Central Community Action Partnership,
  Ofisi ya Twin Falls 208-733-9351 | Ofisi ya Burley 208-678-6514
- **Ukanda 5:** Aid for Friends, 208-254-0290
- **Ukanda 6:** CLUB, Inc., 208-529-4673
- **Ukanda 7:** Our Path Home, 208-336-4663

Pia unaweza kutafuta Kitabu cha Homeless Shelter Directory (Maelezo ya Hifadhi ya Wasio na Makao) mtandaoni kwenye homelessshelterdirectory.org/idaho.html.

***Piga Simu ya Huduma ya Idaho kwa 2-1-1***, taarifa za jamii ya jimbo zima na huduma za rufaa bila malipo kwa mipango inayotoa huduma za afya, binadmau au kijamii.

***Tembelea housingidaho.com au piga simu*** 1-877-428-8844 ili utafute nyumba ya kupangisha inayokidhi mahitaji yako na kiwango cha mapato. Pia kuna zana muhimu kama vile kikokotozi cha gharama ya chini, orodha kaguzi ya nyumba za kupangisha, taarifa za haki na majukumu ya mpangaji.

***Pigia Community Action Partner ya karibu*** kwa 877-375-7382 ili uone mipango iliyopo katika eneo lako ambayo inaboresha ustawi wako kwa jumla, inatoa usaidizi wa chakula na huduma za msingi au kukusaidia kutafuta nyumba. Wabia walioorodheshwa na Ukanda hapa chini:

- **Ukanda 1 na 2:** Community Action Partnership (CAP), 208-746-3351
- **Ukanda wa 3:** Community Council of Idaho (CCI), 208-454-1652, Western Idaho Community Action Partnership (WICAP), 888-900-7361,Metro Community Services (MCS), 208-459-0065
- **Ukanda 4:** South Central Community Action Partnership (SCCAP), 208-733-9351
- **Ukanda 5:** Southeastern Idaho Community Action Agency (SEICAA), 208-232-1114
- **Ukanda 6:** Eastern Idaho Community Action Partnership (EICAP), 208-522-5391
- **Ukanda 7:** El-Ada Community Action Partnership(El-Ada), 208-377-0700

***Pigia Idaho Legal Aid Services*** kwa 208-746-7541 au ***Intermountain Fair Housing Council*** kwa 1-800-717-0695 kwa ajili ya ushauri wa kisheria kuhusu mada zinazohusiana na nyumba.

***Wasiliana na ofisi ya karani wako wa jiji au idara ya polisi ya karibu*** kwa mpango au nyenzo zozote za nyumba katika jamii yako.

## Nyenzo

Nyenzo za jimbo zima zinaorodheshwa kwanza, nyenzo nyingine zote zinaorodheshwa na Ukanda. Rejelea Ramani ya Ukanda kwenye ukurasa wa 3 ikihitajika. **Tafadhali fahamu: Nyenzo na mipango mara nyingi hutegemea vikomo vya ufadhili na matakwa ya ustahiki.*

- **Idaho CareLine:** Piga 2-1-1 au tembelea idalink.idaho.gov
- **Simu ya taarifa kuhusu nyumba:** Piga 877-428-8844.
- **Kwa nyenzo za ziada nenda kwenye:** info.idahohousing.com/homeless-resources
- **Pata nyumba ya kupangisha kwenye:** housingidaho.com
- **Ushauri wa Kodi na Nasaha ya Nyumba:** Piga 877-695-2655 au tembelea finallyhome.org/housing-counseling
- **Ushauri wa Kisheria:** Idaho Legal Aid Services, Inc., 208-746-7541; Intermountain Fair Housing Council, 1-800-717-0695.
- **Nyenzo nyingine:** Matangazo maalum ya eneo, kanisa au makundi ya kijamii, ofisi za jimbo na karani wa kaunti.

Ukanda 1

- **Access Point:** St. Vincent De Paul of North Idaho, 208-664-3095.
- **Community Action Partnership:** Community Action Partnership (CAP), 208-746-3351.
- **Mamlaka ya Nyumba ya Kanda:** IHFA Coeur d'Alene Branch Office, 208-762-5113.
- **Hifadhi ya Dhuluma za Nyumbani:** Safe Passage, 208-644-9303.

Ukanda 2

- **Access Point:** Sojourners' Alliance, 208-310-4554.
- **Community Action Partnership:** Community Action Partnership (CAP), 208-746-3351.
- **Mamlaka ya Nyumba ya Kanda:** IHFA Lewiston Branch Office, 208-743-0251.
- **Hifadhi ya Dhuluma za Nyumbani:** Alternatives for Violence of The Palouse, 877-334-2887; YWCA of Lewiston-Clarkston, 208-746-9655.

Ukanda wa 3

- **Access Point:** CATCH of Canyon County, 208-495-5688.
- **Community Action Partnership:** Community Council of Idaho (CCI), 208-454-1652, Western Idaho Community Action Partnership (WICAP), 888-900-7361;Metro Community Services (MCS), 208-459-0065.
- **Mamlaka ya Nyumba ya Kanda:** Southwestern Idaho Cooperative Housing Authority, 208-585-9325; Wilder Housing Authority, 208-482-7750; Marsing Housing Authority, 208-896-4169; Caldwell Housing Authority, 208-459-2232.
- **Hifadhi ya Dhuluma za Nyumbani:** Hope's Door, 208-459-4779; Rose Advocates, 208-414-0740; Elmore County Domestic Violence Council, 208-587-3300.

Ukanda 4

- **Access Point:** South Central Community Action Partnership, Twin Falls 208-733-9351, Burley 208-678-6514.
- **Community Action Partnership:** South Central Community Action Partnership (SCCAP), 208-733-9351.
- **Mamlaka ya Nyumba ya Kanda:** IHFA Twin Falls Branch Office, 208-734-8531; Twin Falls Housing Authority, 208-733-5765; Blaine County Housing Authority, 208-788-6102.
- **Hifadhi ya Dhuluma za Nyumbani:** Voices Against Violence, 208-733-0100; The Advocates, 208-788-4191; Crossroads Harbor, 208-430-4357.

Ukanda 5

- **Access Point:** Aid for Friends, 208-254-0290.
- **Community Action Partnership:** Southeastern Idaho Community Action Agency (SEICAA), 208-232-1114.
- **Mamlaka ya Nyumba ya Kanda:** Housing Alliance & Community Partnerships, 208-233-6276; American Falls Housing Authority, 208-226-5262; IHFA Idaho Falls Branch Office, 208-522-6002.
- **Hifadhi ya Dhuluma za Nyumbani:** Family Services Alliance, 208-251-4357; Bingham County Crisis Center, 208-681-8712; Oneida Crisis Center, 208-766-3119.

Ukanda 6

- **Access Point:** CLUB, Inc., 208-529-4673.
- **Community Action Partnership:** Eastern Idaho Community Action Partnership (EICAP), 208-522-5391.
- **Mamlaka ya Nyumba ya Kanda:** IHFA Idaho Falls Branch Office, 208-522-6002.
- **Hifadhi ya Dhuluma za Nyumbani:** The Mahoney House, 208-940-0600.

Ukanda 7

- **Usaidizi wa Kufukuzwa kwenye Nyumba/Kodi ya Nyumba:** Jesse Tree, 208-383-9486.
- **Access Point:** Our Path Home, 208-336-4663.
- **Mamlaka ya Nyumba ya Kanda:** Boise City/Ada County Housing Authority, 208-345-4907.
- **Hifadhi ya Dhuluma za Nyumbani:** Women's and Children's Alliance, 208-343-7025.
- Mwongozo wa Mfukoni wa Downtown Boise Resource